Mamujee
PRODUCTS

*Manufacturers of cosmetics, baby products allied chemicals and plastics*

Eckenford Ave / Mkwakwani Road, P.O. Box 394 , Tanga. TanzaniaEmail: mamujee@kaributanga.comTel: +255 27 2646103 / 2647618 Fax: +255 27 2647615 / 2643359.

21st May, 2013

Kwa Ndugu Edna Hamis Danga,

**YAH: WITO WA KUREJEA KAZINI**

Rejea kichwa cha habari hapo juu.
Utakumbuka kuwa ni miaka yapata mitatu tangu ulipopata ajali katika eneo la kazi, ajali iliyotokea mwezi Mei, 2010, muda wote huo kampuni imekuwa ikigharimia matibabu yako ikiwa ni pamoja na gharama za usafiri wa kwenda na kurudi Hosopitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) pamoja na kukulipa mshahara wako wote kwa muda wote huo.

Uongozi wa Kampuni unakuita urejee kazini kutokana na kwamba ripoti ya mwisho ya tathmini ya hali yako ya afya kutoka Hospitali ya Muhimbili pamoja na Idara ya kazi imeshatoka.

Ni matarajio yangu kuwa utatii na kutekeleza wito huu ndani ya muda usiozidi siku tano (5).

Kumbuka: Utafanya kazi zitakazoendana na hali yako ya ulemavu uliyo nayo (light duties).

Wako,

MUHIRI JEREMIA
AFISA UHUSIANO

Nakala. Labour Officer,
Tanga.

KNY AFISA KAZI (M)
S. L.
TANGA